OFISI YA MWANASHERIA
MKUU WA SERIKALI

# OAG MAGAZETINI NA MITANDAONI WIKI HII

10/10/2025 ► 17/10/2025

OAG



# MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI MHE. HAMZA S. JOHARI AKIZUNGUMZA KWENYE MKUTANO WA WADAU WA MAHAKAMA YA TANZANIA

THE GUARDIAN
17/10/2025

# AG's Office berates state legal officers on contracts

By Francis Kajubi

PUBLIC institutions must prioritize meticulous contract management to safeguard national investments, avoid costly legal disputes and ensure the government receives its deserved share of revenues and dividends.

Samwel Maneno, the deputy attorney general, in an address to state attorneys at the opening of a two-day strategic engagement meeting at the Julius Nyerere Leadership School in Kibaha, Coast Region.

Failures in contract oversight have led to unnecessary legal disputes and massive financial penalties for the state, he stated, unde lining that contract management a critical area for the Attorney Ge eral's (AG) Office.

The office is concerned with th sheer volume of agreements th central government handles as an average of 20,000 contracts a entered in each financial year. Th needs great caution to avoid leg disputes, he emphasized.

The government enters into lon term and short-term contracts wi some agreements having lifespa of up to 40 years, straddling va ous phases of government, th demanding thorough, collaborati monitoring by responsible legal o

TURN TO PAGE

## AG's Office berates state legal officers on contracts

FROM PAGE 1

ficers, he said.

"We have learned from our findings that absence or delay in extending urgent professional advice for short and long-term contracts has led to unnecessary legal disputes with investors that must come to an end," he explained.

Remedy is being sought by developing links with the National e-Procurement System that enables the AG's office and heads of institutions to verify contract implementation, thus legal officers need to avoid bureaucracy, embrace technology and focus on results-based performance in legal service delivery.

The meeting examined the position of key state legal stakeholders and their role in safeguarding public investment, coordinated by the Office of the Treasury Registrar (OTR).

Nehemiah Mchechu, the registrar, stressed strict contract management in view of explosive growth in the government investment portfolio, which requires closer contract management to avoid legal disruptions.

Ally Possi, the solicitor general, affirmed the need to strengthen contract management, particularly in public-private partnerships (PPPs), as public institutions have a core responsibility to generate dividends and support national economic growth.

Onorius Njole, the chief parliamentary draftsman, pointed out that achieving a $1trn economy as envisaged in Vision 2050 largely depends on the strength of public institutions, urging a robust legal framework that keeps pace with economic realities.

"Public entities must be governed by investment laws that align with current needs. The legal framework must match the pace of investment growth within public corporations," he declared.



oagtanzania
www.oag.go.tz

HABARI KITAIFA & TANGAZO

MIKATABA

# Serikali kulinda maslahi ya taifa mikataba ya umma

Na Restuta James, KIBAHA

SERIKALI kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa kushirikiana na taasisi za sheria imeanza mchakato maalum wa kuhakikisha mikataba yote ya umma inalinda kikamilifu maslahi ya taifa na kuzuia mianya ya unyonyaji wa kiuchumi.

Hatua hiyo inalenga pia kuimarisha mchango wa mashirika ya umma katika uchumi wa taifa kwa kuhakikisha yanafanya kazi kwa ufanisi na kuchangia angalau asilimia 10 ya mapato yake kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Akifungua kikao kazi cha pamoja kati ya Ofisi ya Msajili wa Hazina, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria, kilichofanyika mjini Kibaha, Pwani jana, Msajili wa Hazina, Nehemiah Mchechu, alisema mkutano huo ni sehemu ya utekelezaji maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu kuboresha mifumo ya sheria na mikataba ili iendane na mwelekeo wa Dira ya Taifa 2050.

"Kama nchi tunafanya biashara na wadau wa ndani na nje, na wakati mwingine migogoro hutokea. Hivyo, tumekutana kuhakikisha mawazo ili kuhakikisha mikataba yetu inalinda maslahi ya Watanzania," alisema Mchechu.

Alisisitiza kuwa maeneo yanayohusisha sheria na mikataba ndiyo yenye hatari kubwa ya upotevu wa fedha, lakini pia yanaweza kuwa chanzo kikubwa cha kuokoa rasilimali endapo yatawekewa mifumo thabiti ya usimamizi.

"Ofisi hizi zote zina wajibu wa 'kupika' sheria na mikataba bora itakayohakikisha uwekezaji unakuwa na tija. Ushirikiano wetu utasaidia kupunguza migogoro na kulinda uchumi wa nchi," aliongeza.

Mchechu aliwataka mawakili wa mashirika ya umma kuwa na mawasiliano ya karibu na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuhakikisha nyaraka zote za mikataba zinapitia mchujo wa kisheria kabla ya kutiwa saini.

Vilevile, aliagiza mashirika hayo kuongeza uzalishaji bidhaa na huduma, kupunguza matumizi yasiyo ya lazima, kudumisha nidhamu ya kazi na kujiwekea malengo yanayopimika ili kuongeza mchango wake kwa taifa.

Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Samwel Maneno, alisema serikali inatazama upya mifumo yote ya kisheria ili kuhakikisha inalingana na dira ya maendeleo ya mwaka 2050 na inalinda maslahi ya Watanzania dhidi ya wawekezaji wasio waaminifu.

"Kutia saini mikataba ni jambo moja, lakini ni muhimu zaidi kuhakikisha masharti yake yanatekelezwa kwa ufanisi mpango wa serikali wa muda mrefu. Tunapitia kila kipengele kabla ya saini ili kuhakikisha hakuna upungufu unaoweza kugharimu nchi," alisema Maneno.

Aliongeza kuwa serikali imeweka mkazo mkubwa katika kuvutia uwekezaji wa kimkakati kwenye sekta za nishati, miundombinu, viwanda na teknolojia, sekta ambazo zinahitaji mifumo imara ya kisheria na usimamizi makini wa mikataba.

"Kwa sasa serikali inaingia katika zaidi ya mikataba 15,000 hadi 20,000 kila mwaka. Tumetengeneza mfumo wa kidijitali unaoungantshwa na NeST (Mfumo wa Ununuzi wa Umma), utakaowezesha kufuatilia mikataba yote kuanzia hatua ya ununuzi hadi utekelezaji," alibainisha.

Maneno alisema mfumo huo mpya utakaorahisisha wakati wa taasisi na wakurugenzi wote wa mashirika kusoma, kuelewa na kutoa taarifa kwa AG kabla ya mikataba kutiwa saini, hatua itakayopunguza migogoro na ucheleweshaji miradi.

Hata hivyo, alionya baadhi ya taasisi za umma ambazo zimekuwa zikiomba ushauri wa kisheria bila kuambatanisha taarifa kamili, akisema hali hiyo imekuwa inasababisha ucheleweshaji uamuzi sahihi.

"Baadhi ya taasisi huandika maelezo mepesi yasiyo na kina. Taarifa sahihi ndizo zinazowezesha uchambuzi wa kina na utoaji ushauri wa kitaalamu unaozingatia sheria," alisema.

Wakili Mkuu wa Serikali, Dk. Ally Possi, na Mwandishi Mkuu wa Sheria, Onorius Njole, wote walisisitiza kuwa mkakati huo wa pamoja ni nguzo muhimu katika safari ya kufikia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 bila migogoro ya kisheria.

Moja ya shabaha za Dira 2050 ni kuchochea ukuaji wa Pato la Taifa kutoka Dola za Marekani bilioni 88.4 sasa mpaka Dola trilioni moja ifikapo mwaka 2050.

Kufikia lengo hilo, serikali imesema ni lazima iendelee kutengeneza mazingira mazuri ya biashara yatakayowezesha taasisi za umma kufanya vizuri kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Kwa sasa, Ofisi ya Msajili wa Hazina inasimamia jumla ya mashirika 308, yakiwamo zaidi ya 252 yanayomilikiwa na serikali kikamilifu, pamoja na mengine ya ubia.



Msajili wa Hazina, Nehemiah Mchechu



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

## MIAKA 26 YA KUMBUKIZI YA BABA WA TAIFA
MWALIMU JULIUS KAMBARAGE NYERERE

Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Hamza S. Johari kwa niaba ya Menejimenti na Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan na Watanzania wote katika kumbukizi ya miaka 26 ya kifo cha Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Baba wa Taifa, Hayati Mwl. Julius Kambarage Nyerere.

*Tutaendelea kumuenzi kwa kufanya kazi kwa Weledi na Ubora ili kulijenga Taifa letu*

**Mwalimu Julius K. Nyerere**
**1999 - 2025**




Hayati Mwl. Julius Kambarage Nyerere
Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

"Weledi na Ubora"

@oagtanzania   Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali   Mwanasheria Mkuu TV   www.oag.go.tz
Kwa msaada wa huduma za kisheria Piga simu bure 0800 11 0188

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA


OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

# MIAKA 26 YA KUMBUKIZI YA BABA WA TAIFA

## MWALIMU JULIUS KAMBARAGE NYERERE

Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Hamza S. Johari kwa niaba ya Menejimenti na Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, anaungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan na Watanzania wote katika kumbukizi ya miaka 26 ya kifo cha Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Baba wa Taifa, Hayati Mwl. Julius Kambarage Nyerere.

***Tutaendelea kumuenzi kwa kufanya kazi kwa Weledi na Ubora ili kulijenga Taifa letu***




**Mwalimu Julius K. Nyerere**

**1999 - 2025**

"Weledi na Ubora"

@oagtanzania Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mwanasheria Mkuu TV www.oag.go.tz

Kwa msaada wa huduma za kisheria Piga simu bure 0800 11 0188

Hayati Mwl. Julius Kambarage Nyerere
Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

# Sheria za mashirika kumulikwa kuendana na uwekezaji

Imani Makongoro, Mwananchi
imakongoro@mwananchi.co.tz

**Kibaha.** Wadau wakuu wa sheria serikalini wamejadiliana namna kufanya mageuzi ya kisasa katika mifumo ya kisheria inayosimamia uwekezaji katika taasisi za umma.

Wamebainisha namna sheria zilizopitwa na wakati na usimamizi dhaifu wa mikataba vinavyoweza kuhatarisha thamani ya uwekezaji wa umma unaokua haraka.

Kwa sasa, thamani ya uwekezaji wa mashirika ya umma nchini imeongezeka na kufikia Sh92 trilioni ikilinganishwa na Sh86 trilioni mwaka uliopita.

Wakizungumza katika kikao kazi cha siku mbili kilichoanza jana kilichohusisha Ofisi ya Msajili wa Hazina, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria, wadau hao wameshauri kufanyika maboresho ya sheria zinazoyaongoza mashirika ya umma, ambazo walisema nyingi haziendani na kasi iliyopo.

Katika kikao kazi hicho kilichokuwa na kaulimbiu: "Nafasi ya taasisi kuu za kisheria za Serikali katika kulinda uwekezaji wa umma" suala la huduma kwa wateja katika taasisi za umma pia lilijadiliwa.

Mwandishi Mkuu wa Sheria, Onorius Njole ameeleza umuhimu wa kufanya maboresho ya sheria zinazoyaongoza mashirika ya umma, akionya mengi kati ya mashirika hayo yameanzishwa chini ya sheria ambazo haziendani tena na dira ya maendeleo ya sasa au ya baadaye ya Taifa.

"Taasisi nyingi ziliundwa miongo kadhaa iliyopita na bado zinaendeshwa kwa sheria za zamani ambazo hazina uhalisia na uchumi wa sasa wala matarajio ya miaka 20 hadi 25 ijayo," alisema.

Njole amesisitiza kikao kazi hicho kuweka mikakati mahususi kuhakikisha taasisi hizo zinajengwa juu ya msingi imara ya kisheria.

Alisema mfumo wa kisheria wa Tanzania unapaswa kuendana na kasi ya uwekezaji wa umma na mageuzi ya utawala bora wa kampuni.

"Huenda mfumo wetu wa sasa wa kisheria haujaendana na kasi ya mashirika ya umma, Msajili wa Hazina (Nehemiah Mchechu) ameeleza maeneo ya changamoto, hatuna budi kuzifanyia suluhisho," alisema.

## Sh92 trilioni

**Thamani ya uwekezaji uliokwishafanyika nchini, ambao unahitaji ulinzi wa kisheria ikilinganishwa na Sh86 trilioni mwaka uliopita.**

Alisema kikao kazi hicho ni fursa muhimu kuoanisha mikakati ya Serikali kuhusu mwelekeo wa uwekezaji wa umma.



Baadhi ya washiriki wa kikao kazi kilichohusisha Ofisi ya Msajili wa Hazina, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria, wakiwa katika mkutano uliofanyika Kibaha mkoani Pwani jana. **Na Mpigapicha Wetu**

Wakili Mkuu wa Serikali, Dk Ally Possi, amesisitiza umuhimu wa kuwa na mifumo ya kisasa ya usimamizi wa mikataba ili kuzuia migogoro ya kisheria na kulinda mali za Serikali.

"Sehemu kubwa ya kesi za Serikali zinahusiana na mashirika ya umma. Hii inamaanisha tunapaswa kuimarisha uwezo wa kitaalamu na kuhakikisha mikataba inasimamiwa kwa kutumia zana za kisasa na utaalamu wa hali ya juu ili kupunguza hatari na hasara," alisema.

Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Samwel Maneno, ameonya kuhusu usimamizi hafifu wa mikataba, akisema unaweza kuchelewesha au hata kuhujumu utekelezaji wa miradi ya Serikali.

"Ikiwa usimamizi wa mikataba utakuwa dhaifu, malengo ya Serikali yatacheleweshwa au kushindwa kabisa kutekelezwa, hii itasababisha hata migogoro isiyo ya lazima," alisema.

Amezungumzia mikataba inayosainiwa katika kila mwaka wa fedha, akisema ni kati ya 15,000 na 20,000, hivyo ufuatiliaji wake unahitaji usaidizi wa teknolojia.

"Tunaweka msisitizo zaidi katika kutumia mifumo ya kidijitali kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa mikataba," alisema.

Msajili wa Hazina, Mchechu, alisema Tanzania kwa sasa inasimamia zaidi ya taasisi za umma 300, ambayo ni ishara ya kupanuka kwa wigo wa mashirika ya umma katika sekta muhimu kama nishati, usafirishaji na fedha.

Alisema mapato ya Sh1.028 trilioni yaliyokusanywa mwaka huu kupitia gawio na michango kutoka taasisi za umma yanaonyesha kuimarika kwa utawala bora na usimamizi wa utendaji.

Mchechu amebainisha changamoto zilizopo katika kuongeza mchango wa taasisi za umma kwenye uchumi na kupunguza utegemezi kwa fedha za Serikali akieleza.

# Serikali yaahidi wawekezaji sheria rafiki

**Na Mwandishi Wetu, Kibaha**

SERIKALI imeeleza dhamira yake ya kutengeneza sheria rafiki za uwekezaji zitakazoiwezesha kufikia uchumi wa kati wa juu kama ilivyobainishwa kwenye Dira 2050.

Moja ya shabaha za Dira 2050 ni kuchochea ukuaji wa Pato la Taifa kutoka $88.4 billioni ya sasa mpaka $1Trilioni itakapo mwaka 2050.

Kufikia lengo hilo, Serikali imesema ni lazima iendelea kutengeneza mazingira mazuri ya biashara yatakayowezesha taasisi za umma kufanya vizuri kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Hayo yalisemwa Alhamisi, Oktoba 16, 2025 wakati wa kikao kazi kati ya Ofisi ya Msajili wa Hazina, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria, kilichofanyika Kibaha, mkoani Pwani.

Msajili wa Hazina, Nehemiah Mchechu alisema maagizo waliyopewa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ni uboreshwaji wa sheria ili ziendane na maono yaliyomo kwenye Dira 2050.

"Tunapaswa kuwa na sheria ambazo zitaongeza utanisi wa taasisi za umma. Tunapaswa kuwa na sheria ambazo zitatoa wigo kwa sekta za umma kufanya kazi kwa ukaribu na sekta binafsi," alisema Mchechu.

Alisema kuongezeka kwa utanisi wa sekta za umma, kutapelekea ongezo la mchango wake kwenye mapato ya ndani ya serikali kutoka asilimia nne ya sasa mpaka kufikia kumi miaka minne ijayo, kama ilivyoelekezwa na Rais Samia.

"Tunapaswa kuboresha huduma na bidhaa zetu, pamoja na kupunguza matumizi yasiyokuwa ya lazima, ili kuongeza mapato na hatimaye gawio kwa Serikali," alisisitiza Mchechu.

Serikali inataka kuona tija katika uwekezaji wake wa sh. 92.3 trilioni ilioufanya katika taasisi za umma na kampuni ambazo ina umiliki wa hisa chache.

Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Samwel Maneno alisema kuwa uimara wa taasisi za umma na sekta binafsi unategemea ubora wa sheria zinazosimamia uwekezaji.

Alieleza kuwa usimamizi wa mikataba ya uwekezaji usipokuwa mzuri, itakuwa ngumu au itachukua muda mrefu kufikia matarajio yaliyowekwa na serikali.

"Aidha, hali hii inaweza kuibua migogoro na hivyo kupelekea kuwakatisha tamaa wawekezaji," alisema huku akibainisha kuwa serikali haiko tayari kufikia hatua hiyo.

"Eneo hili la usimamizi wa mikataba tunalipa kipaumbele kikubwa. Kwa mwaka mmoja wa fedha tunaweza kusimamia kati ya mitaba 15,000 na 20,000.

"Na ili kufanya usimamizi wa mikataba hii uwe wa utanisi, tumeona haja ya kukumbatia matumizi ya teknolojia ili kurahisisha ufuatiliaji."

Aidha, alieleza haja ya kuepuka urasimu usiokuwa wa lazima ili wawekezaji, hasa katika eneo la ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP).

Kwa upande wake Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Ally Possi, alisema sheria za nchi hazitakiwa ziwe kikwazo kwa wawekezaji, badala yake kivutio.

"Ili ndoto yetu ya kuwa na uchumi unaofikia $1 trilioni, ititie, tunapaswa kuendelea kutengeneza mazingira rafiki ya biashara yatakayovutia wawekezaji zaidi," alisema.

Sanjari na hilo, Dkt.. Possi alisema nchi inapaswa kuendelea kuboresha usimamizi wa mikataba, hususani katika eneo la PPP.

Aidha, alisema taasisi za umma zina jukumu la kutoa gawio na kukuza Uchumi wa nchi.

"Lakini hili haliwezi kutimia ikiwa taasisi hizo zitagubikwa na kesi ambazo zitazilazimu kulipa fedha baada ya hukumu ya mahakama kutolewa, na ni katika muktadha huo tumekutana kujadili namna bora ya kukabiliana na mapungufu ya kisheria," alihitimisha Dk. Possi.

Naye Mwandishi Mkuu wa Sheria Bw. Onorius Njole alisema kufikia Uchumi wa $1 trilioni unategemea uimara wa taasisi za umma na ndio maana ipo haja ya kuwa na mfumo imara wa kisheria katika eneo la uwekezaji.

"Ni lazima mashirika ya umma yasimamiwe na sheria za uwekezaji ambazo zinaendana na mahitaji ya sasa," alisema.

"Mfumo wa sheria lazima uendane na kasi ya ukuaji wa uwekezaji katika mashirika ya umma."

# Waomba sheria ya uwezeshaji mahakama kidigitali

Na Mwandishi Wetu

MKURUGENZI wa Taasisi ya msaada wa kisheria ya Everlasting Legal Aid Foundation(E.L.A.F) Dkt Khamis Masoud ameomba Serikali kutunga sheria ya Uwezeshaji wa Mahakama za Kidigitali(Judicial Transparency and Digital Access Act) kwa ajili ya kuwezesha wananchi wengi kuweza kufuatilia kesi zenye maslahi mapana kwa nchi. [illegible]

Dkt Masoud alisema [illegible] Dar es Salaam jana wakati akizungumza na waandishi wa habari wakati akieleza mapendekezo kuhusu mahakama za kidigitali.

Dkt Masoud alisema uwepo wa Mahakama ya kidigitali kutachochea [illegible]

[illegible]

Michuzi Blog | MICHUZI TV
This Space can Only be yours
Call us today on +255 754 271 266



# NAIBU MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI AFUNGUA KIKAO KAZI CHA TAASISI ZA KISHERIA

MICHUZI BLOG · AT THURSDAY, OCTOBER 16, 2025 · HABARI,

Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Samwel M. Maneno, amesema serikali imejipanga kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi zake za kisheria ili kuongeza ufanisi wa utendaji na kuchochea ukuaji wa uchumi wa taifa.

Mhe. Maneno alitoa kauli hiyo leo wakati wa ufunguzi wa kikao kazi cha taasisi za kisheria kinachofanyika mjini Kibaha, mkoani Pwani, ambacho kimeandaliwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria.

Amesema kikao hicho ni sehemu ya juhudi endelevu za Serikali kuhakikisha mashirika ya umma yanafanya kazi kwa ufanisi na kufuata misingi ya sheria, uwajibikaji na weledi, kwa lengo la kufanikisha Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025/2030.

"Tunataka kuhakikisha kila shirika la umma linafanya kazi kwa ufanisi, kwa kufuata misingi ya sheria na weledi, ili mchango wao uweze kuonekana katika maendeleo ya taifa," amesema Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Kwa upande wake, Msajili wa Hazina, Nehemiah Mchechu, amesema Serikali inataka mashirika ya umma kujiwekea mikakati madhubuti itakayowezesha kuongeza mapato, kupunguza utegemezi wa bajeti ya serikali na kuchochea ukuaji wa uchumi wa nchi.

Naye Wakili Mkuu wa Serikali, Dk. Ally Posi, amesisitiza umuhimu wa mashirika ya umma kuwekeza katika teknolojia na ubunifu ili kuongeza ufanisi na ushindani katika soko la kimataifa.



Fullshangwe blog
CONTACT:
phone: +255 713 410 676
+255 755 333 372
P.O BOX 78392, Dar es Salaam
Email. johnbukuku@gmail.com




MCHANGANYIKO

## OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI NA PURA KUIMARISHA UHUSIANO


John Bukuku · 2 days ago
Last updated: 2025/10/15 at 11:00 AM


Share



Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imekusudia kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa uweledi na ubora, ikiwa ni pamoja na kuishauri Serikali juu ya namna ya kuboresha utendaji kazi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), ili kuhakikisha inatoa huduma bora kwa wananchi na wadau waliowekeza katika sekta ya mafuta na gesi.

Akizungumza leo, Oktoba 15, 2025, wakati akifungua mafunzo ya siku tano ya kuwajengea uwezo Mawakili wa Serikali, yaliyofanyika katika Ofisi ya PURA, jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa PURA, Mhandisi Charles Sangweni, amesema kuwa mafunzo hayo ni fursa ya kubadilishana uzoefu kati ya PURA na Mawakili wa Serikali kuhusu utekelezaji wa majukumu ya udhibiti katika Mkondo wa Juu wa Petroli.

Kwa upande wake, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Silinde Gumada amesema kuwa mafunzo hayo yatawasaidia Mawakili wa Serikali kuifahamu kwa undani PURA na namna inavyotekeleza majukumu yake, jambo ambalo litaboresha utendaji wao katika kushughulikia masuala ya kisheria yanayohusu PURA.

oagtanzania




25 1

**oagtanzania** *NAIBU MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI AFUNGUA KIKAO KAZI CHA TAASISI ZA KISHERIA*

Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Samwel M. Maneno, amesema serikali imejipanga kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi zake za kisheria ili kuongeza ufanisi wa utendaji na kuchochea ukuaji wa uchumi wa taifa.

THE RESPONDENT NEWS BUSINESS SPORTS POLITICS TOURISM MEGA MENU

Home > 2025

# Tanzania sets to revamp legal framework to drive Dira 2050

by THE RESPONDENT ONLINE - October 16, 2025 0

Advertisement




By Alfred Zacharia

The government has reaffirmed its commitment to creating investor-friendly laws aimed at propelling Tanzania to upper-middle-income status under the Dira 2050 vision.

Dira 2050 targets increasing the national GDP from around $80 billion today to $1 trillion by 2050.

Achieving this milestone requires a conducive business environment that enables public institutions to operate efficiently while collaborating with the private sector.

The remarks were made on Thursday, October 16, 2025, during a working session in Kibaha, Pwani, which brought together the Office of the Treasury Registrar (OTR), the Attorney General's Office, the Solicitor General's Office, and the Office of the Chief Parliamentary Draftsman.

oagtanzania




34 2 1

**oagtanzania** *OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI YAIMARISHA USHIRIKIANO NA PURA*

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imekusudia kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa uweledi na ubora, ikiwa ni pamoja na kuishauri Serikali juu ya namna ya kuboresha utendaji kazi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), ili kuhakikisha inatoa huduma bora kwa wananchi na wadau waliowekeza katika sekta ya mafuta na gesi.

oagtanzania



# TUPO KARIBU YAKO!

## Tufuatilie kupitia

oagtanzania

info@oag.go.tz

www.oag.go.tz

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali
Mtaa wa Mtumishi
Mji wa Serikali Mtumba
S. L. P 630
Dodoma - Tanzania

**KWA MSAADA WA HUDUMA ZA KISHERIA PIGA SIMU BURE 0800 11 0188**

Weledi na Ubora